

MAMBO YANAYOFANYIKA WAKATI WA UCHAGUZI MKUU

Ibara za 42 (2) na 65 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na kifungu cha 12 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 zinaelekeza kuwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ufanyike kila baada ya kipindi cha miaka mitano (5). Kama ilivyo kwa Nchi nyingine Duniani, katika kuendesha shughuli za Uchaguzi, Tanzania hutumia utaratibu wa Mzunguko wa Uchaguzi ambao umegawanyika katika awamu tatu (3) yaani kabla, wakati na baada ya Uchaguzi kama inavyoonekana katika sehemu ya Mzunguko wa Uchaguzi.

IDADI YA CHAGUZI ZILIZOFANYIKA NA MIAKA YAKE.

Tume iliendesha na kusimamia Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge kwa mara ya kwanza mwaka 1995 ikiwa katika Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa. Mpaka sasa Tume imeendesha na kusimamia Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge awamu tano (5) tangu kuanzishwa Mfumo wa vyama vingi mwaka 1992.

Chaguzi hizo tano (5) zilifanyika katika kipindi cha miaka mitano mitano kuanzia mwaka 1995, 2000, 2005, 2010 na 2015.